OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARIGITTING

S.L.P 157,
KATESH – HANANG.
MANYARA
02/12/2022

Kumb. Na. GTSS/JINSTR/2023/01

JINA LA MWANAFUNZI

…………………………………………………………………

S.L.P ………………………………………………………

KATESH - HANANG.

Ndugu,

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GITTING MWAKA 2023.

1. UTANGULIZI

   Nafurahi kukuarifu kuwa umechanguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023. Shule ya sekondari Gitting iko umbali wa 29km kaskazini mwa mji mkuu wa wilaya ya Hanang (Katesh) na magharibi mwa mji wa Endasak ulio umbali wa 20KM kutoka Katesh. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 10/01/2023 bila kukosa saa moja kamili asubuhi.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

   2.1 SARE YA SHULE (IFANANE KWA RANGI, MISHONO NA UBORA WAKE)

   Mfano wa kitambaa umeambatishwa na fomu hii kwa upande wa tai, suruali na sketi

   A: SARE ZA WASICHANA

   - Sketi mbili za rangi nyekundu (KREATOR) na kiwe kitambaa cha material namba moja. Sketi ziwe ndefu na zisioneshe maungo,

Kitambaa kiwe kizito. MASHONO NI RINDA BOKSI. AINA YA KITAMBAA NI ISTEM

- Blauzi mbili nyeupe aina ya tetron zenye mikono mirefu.
- Sweta la rangi ya BLUU.
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu wala urembo na vyenye kamba (gidamu)
- Stocking/ soksi ndefu nyeupe.
- Tai ya rangi ya nyekundu, kitambaa sawa na cha sketi, iwe na urefu wa wastani. Isiwe ndefu sana wala fupi sana.
- Raba jozi moja kwa ajili ya michezo.
- Fulana na bukta ya rangi ya manjano kwa ajili ya michezo.
- Sketi fupi nyekundu kwa ajili ya michezo na bukta ya rangi ya manjano.
- Mfuko wa kubeba madaftari na vitabu.
- Wanafunzi wa kiislamu wavae hijabu ya vitambaa vilivyotajwa (sketi ndefu ya rangi nyekundu, shati la mikono mirefu la kitambaa cha tetron na ushungi uwe ulioshonwa wa kitambaa cha tetron na uwe na ukubwa wa kutosha).

B. SARE ZA WAVULANA

- Suruali mbili za rangi kaki zenye mshono wa mistari miwili mbele kila upande (celebrations). Zisiwe mnyonyo au model. Kitambaa kiwe kizito, namba moja. Aina ya kitambaa ni (KREATOR).
- Mashati mawili ya tetron ya mikono mirefu.
- Tai ya rangi kaki sawa na kitambaa cha suruali.
- Raba jozi moja kwa ajili ya michezo.
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu wala urembo na vyenye kamba (gidamu).
- Stocking/ soksi ndefu za kaki jozi mbili
- Bukta ya michezo ya rangi ya manjano na fulana ya michezo ya rangi ya manajano.
- Mfuko wa kubebea madaftari na vitabu.
-

2.2 VIFAA VYA DARASANI, CHAKULA NA MAZINGIRA.

- Kila mwanafunzi aje na madaftari makubwa kumi na moja, kalamu, mkebe wa hisabati, rula, na penseli.

- Kila mwanafunzi aje na mahindi kilo 58 kwa mwaka, maharage kilo 25 kwa mwaka. Pia fedha taslimu Tsh 60,000/= kwa mwaka kwa ajili malipo ya mpishi, kuni, mafuta ya kupikia, sukari, chumvi, vitunguu n.k. fedha ZINALIPWA KWA KAMATI YA CHAKULA YA WAZAZI NA SIO KWA SHULE. WEKA FEDHA KATIKA AKAUNTI NAMBA 41010006298 AMBAYO JINA LAKE NI "KAMATI YA CHAKULA GITTING". NI MUHIMU KULIPA CHAKULA KWA WAKATI ILI KUEPUKA USUMBUFU.

Kila mwanafunzi aje na vyombo vya chakula: sahani ya bati, bakuli la bati na kijiko na awe anavitunza vizuri na katika hali ya usafi wakati wote. Wanafunzi hawaruhusiwi kabisa kushirikiana vyombo wakati wa kula chakula.

- Mwanafunzi aje na rimu (A4) moja.

3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.
    - Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Namba 25 ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake ya Sheria Namba 10 ya mwaka 1995 pamoja na kuzingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya kusimamia Elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- Kuwa na heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wa shule, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ni lazima.
- Ni lazima kuwahi katika kila shughuli ya shule na shughuli nyingine utakazopewa.
- Ni lazima kufahamu mipaka na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwapo ndani na nje ya mipaka hiyo WAKATI WOTE wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Ni muhimu kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparatin).
- Ni lazima kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule kwa ujumla.
- Ni lazima kuvaa sare za shule wakati wote wa masomo na wakati wowote unapotakiwa.
- Ni lazima kuzingatia ratiba ya shule kwa wakati wote.
- Ni lazima kutunza mali za umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukunzwa au kusimamishwa shule.

a. Wizi
b. Uasherati na ushoga.
c. Ubakaji.
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
e. Kupigana au kupigana
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g. Kudharau Bendera ya Taifa.
h. Kuwa Mjamzito/kupata mimba.
i. Kuoa au kuolewa.
j. Kutoa mimba.
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l. Kukataa adhabu kwa makusudi.
m. Kuwa na simu ya mkononi.

3.2 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa shuleni na mwanafunzi.

a. Medical examination form ambayo itajanzwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, hiyo na makosa ya jinai.
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

3.3 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA

---

……………………

NICHOLAUS T. NAKEI

M/MKUU WA SHULE.